**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**MKOA WA KAGERA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO.**


SHULE YA SEKONDARI MUBABA

S.L.P 185

**BIHARAMULO.**

**NAMBA ZA SIMU:**

MKUU WA SHULE: **0755 298 756/ 0658 981 122**

MAKAMU MKUU WA SHULE: **0753 066 919/ 0775 866 919**

MWALIMU MWANDAMIZI MALEZI: **0768 207 572/ 0713 272 420**


**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi………………………………………………………………**

**S.L.P…………………………………………………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUBABA MWAKA …...**

**(i)** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **……. Tunampongeza na tunamkaribisha**.

**(ii)** Shule ya Sekondari Mubaba ipo umbali wa km **83** kutoka makao makuu ya Wilaya

(Biharamulo) na km 12 Magharibi mwa mji mdogo wa **Runzewe** katika Kijiji cha

Mubaba na ipo umbali wa Mita 150 kutoka barabara kuu ya lami iendayo Rwanda na Burundi ukitokea (**Dar/Moshi/Mwanza/Kahama).** Kwa wanaotokea mikoa ya **Kigoma** na **Bukoba** shule ipo umbali wa km 38 mashariki mwa mji mdogo wa **Nyakanazi.**

**(iii)**Muhula wa masomo unaanza tarehe **……** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **…….,** mwisho wa kuripoti ni wiki mbili baada ya shule kufunguliwa.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 1. SARE ZA SHULE

### Sare za Shule (Wavulana).

**(a)**Suruali **Jozi mbili** za rangi ya kijani jeshi (kreta/istim) yenye mifuko miwili pembeni na mmoja nyuma. Pia iwe na marinda manne, mawili upande wa kulia na mawili upande wa kushoto na ifunike kifundo cha mguu. **Angalizo:** Isiwe modal na iwe na pindo (turn up).

**(b)** Shati Jeupe **Jozi mbili** za mikono mifupi zisiwe na urembo wa aina yoyote.

**(c)** Viatu vyeusi **Jozi mbili** vya ngozi vyenye visigino vifupi visivyo na urembo wowote vya kufunga na kamba.

**(d)** Soksi nyeusi ndefu **jozi mbili**.

**(e)** Mkanda mweusi wa ngozi usiwe na urembo wowote.

**(f)** **Sare za michezo**; raba za michezo, bukta na T-sheti (**rangi ya Blue**) tu isiyo na nembo ya klabu yoyote ya mpira wala taasisi yoyote.

**(g)** T-sheti yenye nembo ya shule inayopatikana shuleni kwa Tsh **12,000/=** kwa amyehitaji.

**(h)** Tracksuit ya rangi ya blue yenye michirizi nyeupe mitatu pembeni.

**(i)** Sweta rangi ya kijani jeshi lenye nembo ya shule. Linapatikana shuleni **Tsh 12,000/**= kwa anayehitaji.

**(j)** Tai ndefu ya kijani jeshi yenye mistari nyeupe (pundamilia). Inapatikana shuleni **Tsh 6,000/=** kwa anayehitaji.

**(k)** Suruali ya kushindia ya rangi ya damu ya mzee yenye sifa za sare ya shule.

### Sare za Shule (Wasichana).

**(a)** Sketi **Jozi mbili** za rangi ya kijani jeshi (kreta/istim) isiyo na michirizi yoyote, iwe na marinda makubwa manane (8). Iwe ndefu inayogusa vifundo cha mguu.

**(b)** Shati Jeupe **Jozi mbili** za mikono mifupi zisiwe na urembo wa aina yoyote. **(c)** Viatu vyeusi **Jozi mbili** vya ngozi vyenye visigino vifupi visivyo na urembo wowote vya kufunga na kamba. **(d)** Soksi nyeupe ndefu **jozi mbili**.

**(e)** **Sare za michezo**; raba za michezo, bukta na T-sheti (**rangi ya Blue**) tu isiyo na nembo ya klabu yoyote ya mpira wala taasisi nyingine yoyote.

**(f)** T-sheti yenye nembo ya shule inayopatikana shuleni kwa Tsh **12,000/=** kwa anayehitaji

**(g)** Tracksuit ya rangi ya blue yenye michirizi nyeupe mitatu pembeni.

**(h)** Sweta rangi ya kijani jeshi lenye nembo ya shule, linapatikana shuleni **Tsh 12,000/=** kwa anayehitaji.

**(i)** Tai ndefu ya kijani jeshi yenye mistari nyeupe (pundamilia), inapatikana shuleni **Tsh 6,000/= kwa anayehitaji**

**(j)** MUHIMU: -Tunaomba wazazi muwasaidie watoto kuweka alama za kudumu kwenye Vifaa vyao kwa ajili ya usalama.

**ANGALIZO:**

Nguo tofauti na hizo zilizotajwa hapo juu kipengele (a) – (j) **Hazitakiwi kabisa shuleni.**

**2. MAHITAJI YA TAALUMA.**

**(i)** Madaftari yasiyopungua kumi;

**(ii)** **Ream aina ya** Double A bando Mbili (2) kwa mwaka.

**(iii)** Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

**(iv)** Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology.

**(v)** Scientific Calculator

**MAHITAJI MENGINE MUHIMU YA MWANAFUNZI**

i) Godoro size $2^1/_2$ kwa 6.

ii) Mashuka Jozi 2 rangi light blue, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 light blue.

iii) Kiti na Meza yake. iv) Nguo za ndani za kutosha.

v) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).

vi) Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko. vii) Sabuni ya chooni lita tano (5). viii) Fagio moja (1) aina ya chelewa.

ix) Aje na file aina ya Spring au Folder file.

x) Uongozi wa shule unashauri wazazi wote kuwakatia watoto wao bima na waje nazo shuleni. Kwa ambao hawana bima za afya gharama ya bima ni **Tsh 50,400/=**

xi) Kamusi ya kiingereza (Advanced Dictionary) inapatikana shuleni kwa **Tsh 32,000/=**.
xii) Pia waje na vifaa vifuatavyo kulingana na tahasusi anayosoma kama ifuatavyo;

| | | | |
|---|---|---|---|
| PCM | Reki 1 | Mopper 1 | Jembe 1na mpini wake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| PCB | Softbroom 1 | Hard brush 1 | Jembe 1na mpini wake |
| CBG | Fagio la buibui 1 | Kwanja 1 | Jembe 1na mpini wake |

**MICHANGO MBALIMBALI**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule **NMB A/C N0: 31701200088** jina la account ni **MUBABA SECONDARY SCHOOL** Kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye payslip ya kulipia na kidato anachosoma mwanafunzi.

## 3. SHERIA ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978**, pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo kwa kipindi chote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii, utatakiwa kushika na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule ukiwa ndani na nje ya shule **kwani utakuwa ukiiwakilisha shule popote utakapokuwa. Kutokujua sheria hakutakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua stahiki**.

### (a) TARATIBU NA KANUNI ZA

### SHULE 1. HESHIMA:

Kila mwanafunzi anatakiwa; kwanza kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu wanafunzi wenzake, walimu, wazazi/walezi, wageni, viongozi na watu wote kwa ujumla.

**2. USAFI:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.

**3. RATIBA YA SHULE:**

Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu ratiba ya shule. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa maalum kutoka kwa uongozi wa shule. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na kutii wito (**kengele.) Kutokutii kengele, adhabu kali itatolewa.**

**(b) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE MARA MOJA.**

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Uasherati, ushoga na ubakaji.
3. Utumiaji wa vilevi na dawa za kulevya (mirungi, kuber,bangi, sigara n.k).
4. Kupiga/kupigana/kutoa lugha chafu kwa wanafunzi, walimu au jamii.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
6. Kudharau bendera ya Taifa, nembo ya Taifa, fedha na picha za viongozi.
7. Kusababisha/kubeba/kutoa mimba.
8. Kugoma, kuchochea/kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama shuleni.
9. **Mwanafunzi kumiliki line, chaja au simu ya mkononi na viambata vya simu.**
10. **Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani.**
11. **Kugomea adhabu yoyote halali.**
12. **Kutokufanya mitihani yoyote ya shule bila sababu za msingi wala kibali maalumu kutoka kwa uongozi wa shule.(Midterm, Terminal, Annual, Mock, Joint, n.k).**
13. **Kutokuhudhuria vipindi darasani na sehemu zingine kwa mujibu wa ratiba ya shule.**
14. **Kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi shuleni.**
15. **Kumuona na kumkimbia mwalimu pindi anapokuita.**
16. **Kulala nje ya shule kwa wanafunzi wa hosteli bila kibali maalumu.**
17. **Kuonekana kwenye nyumba za wageni na kumbi za starehe.**

**3. 18. Utoro/kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa.**

**19. Kuoa au kuolewa.**

**20. Kuwa nje ya shule bila sare ya shule au bila ruhusa/kibali maalum kutoka kwa uongozi wa shule.**

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakunamtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**ANGALIZO :A)** ***Mwanafunzi atakayebainika/kukamatwa nje ya eneo la shule bila sare ya shule au ruhusa kutoka kwa uongozi wa shule atatozwa tofali mia moja (100) za saruji zitakazokabidhiwa shuleni, pamoja na adhabu zingine.***

**(c) MAKOSA YAFUATAYO YAKIJIRUDIA YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

1. Utoro wa aina yoyote.
2. Kuchelewa kufika shuleni (baada ya likizo) na katika shughuli mbalimbali za shule.
3. Kutokuvaa sare rasmi ya shule kulingana na ratiba ya shule.
4. Uchafu wa mwili (kutokunyoa ndevu/nywele, kutokuoga, usafi wa sehemu anayolala na kutokutunza mazingira ya shule).
5. kuondoka shuleni wakati wa likizo bila kufuata utaratibu wa shule.

**ANGALIZO**: B)Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vifaa vya umeme kama vile pasi, heater, n.k. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kumiliki redio ya aina yoyote bwenini.

**NB:** Fomu zifuatazo zinatakiwa kurudishwa shuleni zikiwa zimejazwa vizuri.

**(i)** Fomu No1. Vipimo vya afya ya mwanafunzi (Vithibitishwe na Daktari wa Hospitali ya Serikali). Fomu No 2. Mkataba wa kutoshiriki Mgomo, Fujo, Makosa ya jinai. Fomu No 3. Kutojihusisha na Mapenzi na Kutomiliki simu shuleni. Fomu No 4. Kutokwenda nje ya mipaka ya shule bila sare au ruhusa.

**NB:** Mwanafunzi aje na kivuli (Copy) cha cheti cha kuzaliwa.

**Karibuni sana**

..........................................

MKUU WA SHULE
MUBABA SEKUNDAR
Box 135
BIHARAMULO

**ALFRED SWEYA KATOBESI**
Mkuu wa shule

## FORM 01: MEDICAL EXAMINATION FORM

***(To be completed by a medical officer in respect of all form one/form five Entrants)***

**Name of Student: ........................................................ Age: ........ Sex: ........ Form: ........**

Please examine the above named in full as to his/her physical and mental fitness for being able to pursue four years of Secondary school education. The examination should include categories (1-17). In case of an acute or defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.

1. Eye sight..........................................................................................................
2. Heart examination ............................................................................................
3. Blood Pressure...................................................................................................
4. Stool routine..................................C/S..........................................................
5. Urine routine.................................C/S...........................................................
6. Sphilis Test........................................................................................................
7. Chest X-Ray.......................................................................................................
8. T.B Test..............................................................................................................
9. Leprosy...............................................................................................................
10. Hearing..............................................................................................................
11. Speech...............................................................................................................
12. Sickle Cell Test..................................................................................................
13. WBC Total differential......................................................................................
14. OBP incuding ESR.............................................................................................
15. FOB......................................................B/S.......................................................
16. Abdomen............................................................................................................
17. Others.................................................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION**: Example; Physical defects or impairments, infections chronic of family diseases etc.


..........................................................................................................................
..........................................................................................................................
..........................................................................................................................


I certify that the above information is correct according to the medical investigation done.

Signature ……………………………

Designation …………………………

Date ………………………………






**Alfred Sweya Katobesi**

**The School Headmaster**

**FOMU 02: MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

**A: HISTORIA YA MWANAFUNZI**

1. Jina la mwanafunzi………………………………………Tarehe ya kuzaliwa……….

Umri…………Kabila………………………Shule aliyotoka ……………………………..

Mkoa…………………… Wilaya………………………………………………………….

2. Jina la Baba/Mlezi………………………………………Kazi yake…………………..

Anakoishi………………………………… Namba ya simu…………………………….

4. Jina la Mama/Mlezi…………………………………….Kazi yake…………………...

Anakoishi……………………………Namba ya simu……………………………………..

5. Dini…………………………………………………………

**B: TAMKO LA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi……………………………………………………mwanafunzi wa kidato cha

…… Nikiwa na akili timamu na bila kushurutishwa na mtu yeyote, nimesona na kuelewa sheria, kanuni na taratibu za shule, na kwamba nakubali kufunga mkataba huu na kuahidi kwamba sitashiriki katika fujo/mgomo wowote na sitafanya kosa lolote la jinai nikiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Mubaba.

Ninakubali pia kwamba endapo nitafanya mambo mengine yaliyo kinyume na Mkataba huu, hatua za kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Jina la mwanafunzi………………………………………………………………..

Saini…………………………… Tarehe ……………………………………

Jina la Mzazi/Mlezi………………………………………………………………..
Saini…………………………… Tarehe…………………………………….

**C: TAMKO LA MZAZI/MLEZI LA KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE HII.**

Mimi…………...…………………………Mzazi/Mlezi …………………………………..

Ninakubali kuwa mtoto wangu atahudhuria masomo na kuzingatia sheria zilizowekwa kuanzia sasa hadi atakapomaliza kidato cha …………. Mwaka…………… katika shule ya sekondari Mubaba. Aidha ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule ikiwemo sare za shule na mahitaji mengine yaliyoainishwa na

shule. Hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu endapo nitashindwa kumpatia mahitaji ya shule mtoto wangu.

Saini ya Mzazi/Mlezi ………………………………………

Tarehe ……………………………………………………

……………………………

**Alfred Sweya Katobesi**
**Mkuu wa shule**

**FOMU 03: MWANAFUNZI KUTOJIHUSISHA NA MAPENZI PAMOJA NA KUTOMILIKI SIMU/LAINI/CHAJA YA SIMU SHULENI.**

Kikao cha bodi ya shule cha tarehe 23.05.2025 kilikubaliana na adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi atakae kamatwa na simu au viambata vyake, au atakaye kamatwa akijihusisha na mapenzi shuleni: -

1. Kuchapwa **viboko vitatu (3)** mbele ya wanafunzi wote mstarini.
2. Kusimamishwa masomo kwa muda wa **siku ishirini na moja (21).**
3. Siku ya kurudi shuleni Mwanafunzi atatakiwa kuja na Mzazi/Mlezi wake na kwa kushirikiana watalipia faini ya **tofali za saruji mia mbili (200).**
4. Simu na kadi ya simu vitavunjwa mbele ya wanafunzi na mzazi/mlezi.

**N.B:** Endapo mzazi/mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (1- 4) mwanafunzi atafukuzwa shule.

JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………….……...

SAHIHI: ……………………………… TAREHE……………………………..

JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………………….

SAHIHI: ……………………… TAREHE……………………………

**FOMU 04: KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE BILA SARE YA SHULE AU RUHUSA MAALUMU KUTOKA KWENYE UONGOZI WA SHULE.**

Kikao cha bodi ya shule cha tarehe 23.05.2025 kilikubaliana na adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi atakaye kamatwa nje ya mipaka ya shule bila sare ya shule au ruhusa:- 1. Kuchapwa **viboko vitatu (3)** mbele ya wanafunzi wote mstarini.

2. Kusimamishwa masomo **siku kumi na nne (14)**.

3. Siku ya kurudi shuleni mwanafunzi atatakiwa kuja na mzazi/mlezi wake na watakabidhi **tofali hamsini (50) za saruji.**

**N.B:** Endapo Mzazi/Mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (1- 3) mwanafunzi atafukuzwa shule.

JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………………

SAHIHI: ………………………………          TAREHE……………………………

JINA LA MZAZI/MLEZI……………………………………………………………………

SAHIHI: …………………………………   TAREHE…………………………

……………………………

**Alfred Sweya Katobesi**

**Mkuu wa shule**

**SHULE YA SEKONDARI MUBABA**

**Karibuni Sana**